# HOTUBA YA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, MWENYEKITI WA CHAMA CHA MAPINDUZI NA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, WAKATI AKIFUNGA MKUTANO MKUU WA KUMI WA CCM – TAIFA, 8 DISEMBA 2022
## DODOMA

- ***Mhe. Abdulrahman Omar Kinana, Makamu Mwenyekiti wa CCM – Bara;***
- ***Mhe. Dkt. Husein A. Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Makamu Mwenyekiti wa CCM, Zanzibar;***

- ***Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamo Mwenyekiti Mstaafu na Mwenyekiti wa Muda wa Uchaguzi katika Mkutano huu***
- ***Mhe. Makamu wa Rais Philip Isdor Mpango;***
- ***Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Mwenyekiti wa CCM Mstaafu na Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri Muungano wa Tanzania;***
- ***Viongozi wastaafu kutoka Serikali zote mbili; Serikali ya JMT na SMZ;***
- ***Viongozi wastaafu CCM katika nyadhifa zenu tofauti;***
- ***Wazee na wadhamini wa chama;***
- ***Ndugu Waziri Mkuu wa JMT;***
- ***Makamu wa Pili wa Rais wa SMZ;***
- ***Ndugu Daniel Godfrey Chongolo, Katibu Mkuu wa CCM;***
- ***Wageni wetu Mnaowakilisha Nchi na Vyama Rafiki;***
- ***Mabalozi na wawakilishi wa Taasisi za Kimataifa;***
- ***Mama Fatma karume ukiongoza wenza wa Viongozi pamoja na mwenza wa Mwenyekiti wa CCM;***

- ***Viongozi na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa 10 wa CCM taifa;***
- ***Ndugu wanahabari, Vikundi vya burudani, wasanii wetu, wageni waalikwa wote;***
- ***Wana CCM mabibi na mabwana***

**CCM OYEE!**
**MAPINDUZI!**
**KIDUMU CHAMA CHA MAPINDUZI!**

Ndugu zangu nami niongeze sauti yangu kwenye kumshukuru mola Nianze kwa kumshukuru Mola kwa kutuwezesha kukamilisha shughuli zote za Mkutano Mkuu wa Kumi wa CCM-Taifa kwa mafanikio makubwa.

Vile vile mafanikio haya niseme yametokana na kazi nzuri iliyofanywa na Mwenyekiti wa muda …. ambaye, kama ilivyo kawaida yake, ameongoza mkutano wetu wa uchaguzi vizuri sana. Yeye siku zote amekuwa ni kisima cha busara na ushauri kwa Chama chetu na Taifa kwa ujumla. Kwa hivyo, kwa niaba yenu Wajumbe, nataka nimshukuru sana kwa kuendesha uchaguzi wetu vizuri mno.

Ndugu zangu. Nimepokea kwa moyo mkunjufu kazi mlionikabidhi jana ya kuendelea kukiongoza Chama chetu kwa miaka mitano ijayo. Mmeonesha imani mlionayo kwangu ambayo inaaashiria upendo na kuridhika kwenu namna nimekuwa nikikiongoza Chama hiki na taifa kwa ujumla tokea kunikabidhi hatamu za uongozi karibu mwaka wa pili sasa. Sina lugha nzuri zaidi ya kueleza shukrani zangu kwenu ila tu naomba mpokee ASANTE SANA na kwa dhati ya moyo wangu.

Kwa Makamu Mwenyekiti wetu mpya wa CCM na Rais wa Zanzibar, **Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, yeye tayari amekwishatoa shukrani zake mbele yenu kwa kumchagua kushika nafasi hiyo ya uongozi katika Chama chetu. Lakini pia mmetuthibitishia kuwa mna imani nae pamoja na sisi tuliompendekeza kwenu. Nawashukuru! **Ahsanteni sana**.

Lakini napenda nitoe shukrani za kipekee pia kwenu Wajumbe kwa kuturejeshea kwenye uongozi wa Chama chetu kaka yangu **Ndugu Abdulrahaman Kinana.** Nina hakika kwa pamoja tutaenda kushirikiana ili kulinda, kutetea, na kuendeleza malengo na madhumuni ya Chama chetu, Chama Cha Mapinduzi.

Vilevile, ninawashukuru sana wazee wetu wote **Wenyeviti** wa Taifa Wastaafu na **Wenyeviti wa Mikoa ambao hawakuendelea, Wenyeviti wa Jumuiya na Makamu Wenyeviti wa Jumuiya ambao hawakuendelea**, na Makatibu Wakuu Wastaafu pamoja na wote ambao walikuwa kwenye dhamana mbalimbali lakini hawakuendelea kwa kazi nzuri sana waliyoifanya lakini pia kukubali mwaliko wetu wa kuja kuungana nasi hapa, katika shughuli hii muhimu ya ujenzi wa kuimarisha Chama chetu.

Kwa namna ya kipekee ninamshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa CCM-Zanzibar, anayemaliza muda wake, **Dkt. Ali Mohamed Shein**. Tumeshirikiana naye vizuri sana kwa kipindi chote cha **miaka kumi** ya uongozi wake katika Chama na hata pale alipokuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Alikuwa kiongozi makini, jasiri, mnyenyekevu, mwenye hekima na busara. Kwa hakika, ndani ya kipindi

chote cha uongozi wake, **Dkt. Ali Mohamed Shein**, alibeba sifa hizo na kuwa mfano wa kuigwa katika Chama chetu na kwa wengineko.

Tunamuomba Molla wetu Mtukufu, ampe afya njema na kuendelea kuwa miongoni mwa hazina za CCM na pahala pa kuchota hekima na busara zake, kila tutakapozihitaji. Tunamtakia mapumziko mema yaliyojaa furaha, amani na upendo yeye na familia yake, akiwa **Rais na Makamu Mwenyekiti Mstaafu wa CCM - Zanzibar** na mjumbe wa Baraza la Ushauri la Viongozi Wakuu Wastaafu. CCM chini ya uongozi huu mpya itaendelea kumuenzi na kuwa nae kwa karibu sana.

Ninawashukuruni pia Wajumbe wote, kwa ushirikiano wenu mkubwa na umakini mliouonesha wakati wote wa mkutano huu. Shukrani za kipee ziende kwa Wajumbe wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa, chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, **Ndugu Daniel Godfrey Chongolo**, Kamati Tendaji ya Maandalizi ya Mkutano Mkuu, Watendaji wote wa CCM na Jumuiya zake na wengine wote waliohudumia mkutano huu kwa kutupa ulinzi na huduma nyengine zote muhimu, mpaka tukaweza kuifanya vyema kazi iliyotuleta hapa. Tunawashukuru sana.

Na kwa mara nyingine tena ninawashukuru wageni wetu wote waliopo hapa, kutoka ndani na nje ya nchi wanaowakilisha vyama vya siasa na taasisi mbalimbali pamoja na wale kutoka nje ya nchi kwa kukubali mwaliko wetu na kuja kutuunga mkono na kwa salamu za kutia moyo.

Kwa viongozi wote wapya waliochaguliwa katika ngazi mbalimbali napenda kutoa pongezi nyingi na maalum. Chama chetu na Jumuiya zake sasa kimekamilisha kujaza safu zake zote za uongozi wa kuchaguliwa, kuanzia ngazi za Mashina hadi Taifa. Kazi imekamilika, kinachofuata sasa twende tukajenge chama.

Na kwahiyo, kwa dhati kabisa ninapenda kuwashukuru wana-CCM wote waliojitokeza kushiriki kwa kupiga kura au kugombea. Waliojitokeza wengi wazuri na wakati mwingine ilikuwa vigumu kuamua tumchague nani na kumuacha nani; jambo linaloonyesha kuwa tunayo hazina kubwa ya **viongozi**. Kushiriki kwao katika uchaguzi ni hatua muhimu sana katika azma yetu ya kuimarisha Demokrasia nchini, maana hakuna Chama kingine cha siasa kinachoweza kuwa mfano wa Demokrasia kama ilivyo CCM. (***Watani zeyu wako hapa, lakini lazima mkubali kuwa sisi ndio baba lenu, si ndio? Au ndio mama lenu***). Ndiyo maana kila kinachofanywa na CCM, huvutia wengi, kutulia na kuangalia na kuona CCM wanafanya kitu gani.

**Ndugu Wajumbe**

Mwaka huu umeweka rekodi katika Chaguzi zote zinazofanywa ndani ya CCM, mwaka huu ulikuwa na wagombea wengi sana kutoka ngazi zote. Kutoka Shina hadi ngazi za juu.

Kwa hakika, Uchaguzi Mkuu wa CCM na Jumuiya zake wa **Mwaka huu wa 2022** umekuwa na mafanikio makubwa na kielelezo cha kukomaa kwa Demokrasia ndani ya CCM. Umethibitisha kuwa CCM **si mali ya mtu**, bali ni mali ya **wanachama**.

Hata hivyo, tukiri kuwa CCM inaongozwa na wanadamu, **sio malaika**. Hivyo, haiwezi kuwa haina dosari za hapa na pale. Tutaendelea kuimarisha Demokrasia, uwajibikaji kwa uadilifu kwa viongozi kwa kujitathmini mara kwa mara ili tuwe tunarekebisha kasoro zetu kila

zinapotokea. Ni Imani ya Chama chetu kujikosoa na kujisafisha au kukosolewa na kujisafisha.

Kama mlivyoona wakati wa chaguzi zetu, tumejitahidi kupima kila tuhuma, na kila lalamiko; na pale ushahidi ulipodhihirika tumechukua hatua. Kwa kweli tumefanya kazi kubwa ya **kuchuja wagombea**, na bila shaka tumepata **viongozi walio safi**. Kwa bahati mbaya, Kama yupo aliyepenya ambaye si msafi, basi lazima **abadilike** na aanze **kujirekebishishisha**. Vyenginevyo afahamu kwamba, hataweza **kubaki salama ndani ya CCM**.

Waheshimiwa Wajumbe, katika zana ya kujikosoa na kujirekebisha naomba hapa kurekebisha ulimi ulivyoteleza kwa kaka yangu Mzee Makamba wakati ananisifia alisema usiogope hutokufa, mtu mzuri hafi. Hajakusudia kwamba wanaokufa ni watu wabaya. Wote hapa tumefiwa na baba na mama na ndugu na wote walikuwa wazuri.

Kwa hiyo nirekebishe kile kipengee kisiende kikatumika vibaya. Mzee alikuwa kwenye emotion, alidhani amenikosea alivyoniambia si utakufa utatupisha, lakini akanirudisha akaniambia usijali, mtu mzuri hafi. Alikuwa kwenye emotion. Lakini hajakusudia vingine vyovyote.

Kwa hiyo, nirudie kuipongeza sana safu mpya ya viongozi wote wa CCM na Jumuiya zake katika ngazi zote, wakiwemo wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa. Halmashauri Kuu hii mpya pamoja na Kamati Kuu na Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa, tutakazokwenda kuziunda **hapo baadae**. Viongozi wote hawa watabeba dhima na jukumu mahsusi la kuongoza mapambano ya kuleta ushindi kwa CCM, katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa **Mwaka 2024** na Uchaguzi Mkuu wa **Mwaka 2025** pamoja na kukiimarisha Chama chetu katika nyanja zote za maendeleo ya kisiasa na kiuchumi.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu**

Baada ya zoezi la Uchaguzi Mkuu wa **Mwaka huu** kufikia tamati, sasa ni kazi ya kukijenga Chama na kuwatumikia wananchi ili kukiletea au kuliletea taifa maendeleo. Ni wakati wa kuzika tofauti zetu na kwa pamoja tufanye kazi kwa bidii na kwa mtindo mpya ili kukabiliana na mazingira tuliyonayo sasa; kwani kila zama na changamoto zake.

Kwahiyo changamoto tulizonazo sasa ni tofauti na za wakati mwingine wowote. Kwahiyo tuzibadilishe, tuzifanyie kazi changamoto zilizopo ili zilete maendeleo ya taifa

Kama nivyoeleza hivi karibuni kule Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam, kuwa zama zetu hizi zinapitia changamoto nyingi si hapa nchini kwetu tu, bali na duniani kote; na hivyo tujipange vyema kukabiliana nazo. Na kwa mtazamo wangu, nimeona hatuna budi kubuni mbinu mpya kwendana na wakati tulionao katika kujenga Tanzania mpya. Katika kufanikisha hilo na kwa jukumu nililopewa la kuiongoza CCM na Tanzania nimekuja na wazo ambalo limekubalika ndani ya chama changu wazo la dhana ya misingi minne mikuu ya **Maridhiano**, **Ustahamilivu**, **Mabadiliko** na **Kujenga Upya;** au kwa lugha ya Kiingereza ni *4Rs* ninazozungumza kila siku ambazo ni *Reconcilation*, *Resiliency*, *Reforms* na *Rebuilding*.

Ndugu zangu waswahili wanasema ***Isiyo kongwe haivushi***. Kwahiyo tunapofanya kazi zetu lazima tuangalie tunapotoka; na hiyo ndio kongwe yetu, tulipo sasa hivi lakini na tunapokwenda. Kwa maana hiyo ili nilazimu kufanya marejeo. Niliangalia Azimio la Mkutano wa Chama cha Mapinduzi,

hili lilikuwa azimio la Mkutano mkuu wa Taifa mwaka mmoja wa TANU na ASP uliofanyika mwaka 1977 wakati tunaunganisha vyama. Na kwa bahati Azimio hili unalikuta ukifungua tu Katiba ya Chama chetu pale kwenye ukurasa wa Utangulizi. Azimio linatuambia: "***Tumeamua kwa pamoja kuunda chama kipya, kuendeleza mapinduzi ya kijamaa nchini nchini Tanzania na mapambano ya ukombozi wa Afrika juu ya misingi iliyojengwa na TANU na ASP***." Ndio maaana chama chetu hichi cha Mapinduzi kiliundwa kwa misingi hiyo.

Chama tunachokiunda tunataka kiwe chombo Madhubuti katika muundo wake na hasa katika fikra zake na vitendo vyake vya kimapinduzi za kufutilia mbali aina zote za unyonyaji hapa nchini napia kupambana na jaribio lolote lile la mtu kumuonea mtu mwingine, au shirika au chombo, cha nchi kuonea na kudhalilisha wananchi, kudhoofisha uchumi au kudhorotesha maendeleo ya taifa. Tunataka kishike barabara hatamu za shughuli zote za umma kwa maslahi ya wakulima na wafanyakazi wa taifa letu. Tunataka kiwe kiungo cha wanamapinduzi wa Tanzania na wanamapinduzi kokote walipo duniani.

Dhana hii ndugu zangu, inagusa maeneo yote ya maisha ya Mtanzania na binadamu kwa ujumla, kama yalivyoainishwa katika Ilani yetu ya Uchaguzi na Dira za Maendeleo za Taifa. Zaidi dhana hii inatoa msukumo katika utekelezaji wa majukumu manne makuu yaliyo mbele yetu yafuatayo kitaifa na kichama:

**Jukumu la kwanza**: Kuimarisha **umoja** na **mshikamano** wetu na kuelekeza mawazo na nguvu zetu zote kwenye ile kazi kubwa na ya msingi kwa kila chama cha siasa. Tusikubali kabisa mikiki mikiki ya

uchaguzi kuwa chanzo cha mifarakano baina yetu kitaifa na pia kuanzisha **nyufa ndani ya CCM**. Wakati wa uchaguzi, makundi ni mengi, wagombea ni wengi, tutatofautiana lakini tukimaliza tusikubali kujenga nyufa ndani ya chama chetu. Na ndivyo tulivyoelekezwa na lile Azimio la wazee wetu

Uchaguzi ukimalizika lazima makundi yaishe na tuendelee na kazi za kukiimaarisha Chama na ujenzi wa Taifa kwa pamoja. Kwani **umoja ni nguvu**, na **umoja ndio ushindi wetu.**

Sasa wamesema wakubwa zangu hapa, na mimi nataka niseme kidogo kwamba kuna vijinongwa nongwa ndani ya chama chetu vinaendelezwa. Lakini nataka niseme kuwa mwana CCM ambae anakijua Cghama anajua mwelekeo wa Serikali, Sera za Chama anajua mweleko wa Chama chetu au kwa lugha nyingine, kwa wana CCM waliotokana na Chama cha Mapinduzi hawawezi kufanya nongwa wakaharibu chama chao. Lakini kuna wana CCM walioshika nyadhifa tofauti tofauti wakapitia kwa Chama cha Mapinduzi hawa wanaweza kutuharibia Chama.

Hivyo, ninatoa wito kwa viongozi wote wa CCM na Jumuiya zake katika ngazi zote, kuzingatia ukweli huo na sote kwa pamoja tushirikiane na **kupanga** na **kuandaa mikakati** ya utekelezaji wa Ibara ya 5 (1) ya Katiba ya Chama chetu ya Mwaka 1977, Toleo la 2002. Tukumbuke kuwa, **kushindwa kujipanga** ni **tunajipanga kushindwa!** Kwahiyo tusishindwe kujipanga.

Rais Kikwete amesema hapa kushindwa kujipnga ni kujipanga kushindwa naomba tusiende kujipanga kushindwa bali tukajipange kushinda.

**Jukumu la Pili:** Kuimarisha nguvu katika kusukuma kasi ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi ambayo wananchi waliotuweka madarakani, wanatarajia tufanye utekelezaji huu. Kama tunavyofahamu, siku zote mtu anaaminiwa kwa uungwana wake. Na uungwana wa CCM kwa wananchi, ni kutekeleza ahadi zetu kwao, kama zilivyoainishwa katika Ilani tuliyoitangaza. Serikali zilizopo madarakani ni **Serikali za CCM**. Hivyo watendaji wake ndani ya Serikali; Tanzania Bara na Zanzibar, lazima washirikiane, waheshimiane kwa dhati, na kwa kuzingatia mipaka ya madaraka yao na kanuni zetu za kiutawala. Washirikiane kuijenga Tanzania. Tanzania ni Nyumba moja na hatuna nyingine. Lazima pande zote mbili za Muungano tuheshimiane, tushirikiane kujenga Tanzania.

Watendaji wa Serikali wasiogope, na kwa kweli wanalazimika kwenda sambamba na Chama Tawala. Kwa sababu kuwepo kwao ni kwasababu chama hiki kimeweka Serikali. Kama wanatumikia Chama hiki ni lazima watekeleze Ilani ya Uchaguzi ya Chama hiki. Kwa hiyo utekelezaji huo wa Ilani yetu si hiari; bali hili ni **Wajibu** kwa kila mtendaji wa Serikali.

Aidha, uongozi wa CCM katika ngazi zote unao wajibu pia wa kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka **2020 – 2025** katika maeneo yao na kujadili taarifa za Serikali katika ngazi zao kuhusu utekelezaji wa Ilani hiyo. Tumeonesha mfano hapa, tumezijadili kazi za Serikali hapa. Kama kazi kama hii mtaifanya kweny maeneo yenu. Hamtakuja na hoja za kule mkazileta. Tutamalizana kule kule. Hapa au kwenye Halmashauri Kuu yatakuja yale makubwa. Yatakuja yale yaliyoshindikana katika ngazi za Wilaya na ngazi za mikoa. Hivyo basi Viongozi wa Chama, Viongozi wa Serikali muende mkashirikiane. Make mjadili kwa pamoja utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mkuu

wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa ahojiwe kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Na kwa bahati nzuri, nina timu nzuri ya Makamisaa wa Chama cha Mapinduzi katika Mikoa, hilo ndilo jeshi langu. Na mpaka sasa wanakwenda vizuri. Naomba mkajipange vizuri, tengenezeni mipango, kaeni na Chama, jadilini yanayotekelezwa huko, jibuni hoja. Vikiwazidi tuleteeni juu. Lakini jibuni hoja huko chini ili wasije watu wakalalamika hapa kwa mambo ambayo kule tayari yanafanyika. Kwa hiyo nawatakia kazi njema.

Na hii ndio sababu mwanzoni mwa Mkutano huu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ziliwasilisha taarifa zao za utekelezaji wa Ilani. Kwa hiyo, kama nilivyosema, wakuu wote wa Miko ana Wilaya muende mkaendeleze mwendo huu. Jipangieni kama ni miezi mitatu, miine, sita lakini muwasilishe taarifa zenu za utendaji Chamani na Chama kiwahoji. Na chama ngazi ya mkoa ikisema huyu hatumuelewi jua umekwenda na upepo.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu**

**Jukumu la Tatu** linalotukabili ni la msingi sana kwa Chama chetu: kuhakikisha kuwa, CCM **hailali usingizi** wala **kulewa madaraka**. CCM lazima iendelee kuheshimu imani ya wananchi waliotuchagua na kutuweka madarakani na kuwa **viongozi – watumishi.** Tanguliza mbele watumishi kwanza halafu ndio Kiongozi. Tuwatumikie wananchi kwanza kabla ya kutafuta heshima kutoka kwao. Jinsi utakavyotumikia wananchi ndivyo watakavyokuheshimu Heshima ya kweli haitokani na ukubwa, au mabavu au vitisho. Bali ni mavuno baada ya kutumikia watu kwa weledi, **uadilifu** na **unyenyekevu** watakuheshimu.

Ndugu zangu Kama tunavyofahamu, CCM kwa historia yake ni Chama cha **kuwakomboa wanyonge**. Kwa hiyo, Kama ipo sifa ambayo CCM lazima iilinde daima, ni sifa ya kuwa mtetezi **imara wa wananchi wake.** Si kwa maneno bali kwa vitendo.

Tusisahau kuwa, Utawala bora ni utetezi wa haki, kuwajibika kwa wananchi na kuwatumikia, badala ya **kujitumikia wenyewe**. Huko nyuma wananchi waliohisi wanaonewa walikuwa wakikimbilia ofisi za CCM. Walikuwa wanaogopa Polisi na Mahakama. CCM ndio Mkombozi wao. Lakini leo kila mtu ajipime kwenye eneo lake. Amekembiliwa lini na mwananchi. Na mwananchi akienda anampokeaje, anamhudumia vipi. Naomba sana turudishe Imani ya wananchi wetu. Wajue kwamba CCM ndio kimbilio lao.

Ninapenda kuwahakikishia Wana CCM na Watanzania wote kuwa Serikali ya CCM itajiepusha **kulewa madaraka** au **kuyatumia vibaya**. Na nyinyi viongozi wa CCM popote mlipo, nataka muwe macho, ili dalili za kulewa madaraka au kuyatumia vibaya zinapojitokeza, hatua za kusahihisha hali hiyo zichukuliwe **mara moja**. Viongozi wa CCM na tulio Serikalini tuwe **watumishi kwanza,** na viongozi **baadaye**. Nyinyi ni viongozi - watumishi. Mimi mwenyewe ni **kiongozi - mtumishi**. Nipo hapa **kuwatumikia Watanzania wote**, si **kujitumikia mwenyewe**. Asiyekubaliana na hali hiyo, afahamu kuwa, **nafasi** kwa wakati huu ndani ya Chama na Serikali ni ndogo mno. Kama nilivyosema kama umebahatika kupenya lakini huna Imani hii basi jitayarishe, tutakugundua na utatupisha. Sisi sote ni watumishi wa wananachi na hatuna hiari. Lazima tufanye kazi za wananchi kazi ya wananchi kwa bidii, maarifa na uadilifu.

Ndugu zangu, tunazo taasisi za kulinda na kutetea haki za raia. Tunalo Bunge la Jamhuri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mahakama, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Maadili na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Lakini kuwa na taasisi za kusimamia haki za raia ni jambo moja; na usimamizi utekelezaji wa majukumu yaya kusimamia haki za raia ni jambo jengine. Nimegundua kuna kulega lega leaga katika kusimamia haki za raia. Hivyo basi ndani ya Serikali tumeamua kuunda timu itakayofanya mapitio katika Taasisi hizo kuleta mapendekezo na kufanya marekebisho ya yatakayopendekezwa.

Sisi ni taifa huru; raia wetu ni lazima wawe huru. Sisi ni taifa linalopenda kuheshimiwa; Serikali zetu nazo ni lazima ziwaheshimu raia wake. Na kwa Watanzania wote wanaonisikiliza napenda kuwahakikishia kuwa tutasimamia haki zao zilizoahidiwa kikatiba. Si vyema kwa raia wa nchi hii kunyanyaswa, kuonewa au kudhulumiwa na mamlaka za dola.
Ndugu zangu, hili ni jikumu zito na lazima tusaidiane. Kwasababu mengine haya yanatokea kwenye ngazi zenu na siis tullio juu hatuyaoni. Na ndio mana nikasema Chama na Serikali muende mkafanye kazi pamoja. Yanapotokea hayo, chama kijue, Serikali ijue. Au Chama kama kinajua wafanye na Serikali na yenyewe ijue ili hatua zichukuliwe.

Aidha, kama nilivyowahi kueleza mara nyingi huko nyuma, leo pia napenda kurejea **nia** na **azma** yangu ya kuendeleza utamaduni na kusimamia wa majadiliano ya kiungwana baina ya Vyama vya Siasa, kwa lengo la kuimarisha misingi ya kidemokrasia, Umoja na **Maridhiano ya Kitaifa** katika nchi yetu, na kuondoa mawazo potofu kuwa, Demokrasia ni Tume ya Uchaguzi na uchaguzi tu. Demokrasia ni zaidi ya hapo. Na

muhimu zaidi kujenga utamaduni wa Demokrasia, ambao ni zaidi ya **uchaguzi** na **taasisi za kusimamia uchaguzi**. Demokrasia ni utamaduni, si wa taasisi wala si taratibu za uchaguzi peke yake. Lakini Demokrasia ni jinsi ya kuendesha mambo yetu nchini kwetu, kwa mazingira yetu na jinsi ya rasilimali tulizonazo. Hiyo ndio demokrasia. Kushirikishana watanzania wote. Na kuendeleza mambo yetu katika misingi hiyo.

Kwa sababu hiyo, Serikali na vyama vya siasa wote kwa pamoja wanao wajibu wa kukuza utamaduni wa kuheshimiana, kuvumiliana, na kushirikiana kwa mambo yenye maslahi kwa taifa na wananchi. Utamaduni huo pia unapaswa kupenyezwa kwenye nyanja zote za maisha ya mahusiano baina ya raia, na baina ya jamii mbalimbali.

Vile vile, ni muhimu pia kwa **vyama vya upinzani** hapa nchini, kuelewa kuwa, utaratibu huo wa majadiliano tuliouanzisha **hautuvui** sisi CCM dhamana yetu tuliyopewa na wananchi ya kuwa **Chama Tawala**.
Utamaduni huu, unatufanya sisi CCM ambao ni Chama Tawala, kuvuta wenzetu tukae tujadiliane, tukubaliane, jinsi ya kuendesha siasa zetu kwa utulivu na kwa ustaarabu. Jinsi ya kuendesha mambo yetu. Lakini bado tunabaki kuwa chama tawala. Na tuna dhamana tuliopewa na wananchi. Dhamana ambayo tutaienzi na kuilinda. Hivyo, ninawaomba viongozi wa vyama hivyo nao waelewe hivyo; wasisahau kuwa sisi ndio wenye dhamana ya kuongoza nchi. Na dhamana hiyo hatukujipa, bali tumepewa na wananchi.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu**
**Jukumu la Nne** linatokana na Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kumi wa CCM-Taifa, ni maazimio yaliyowasilishwa na Kamati ya Maazimio kabla ya

uchaguzi. Bila shaka maazimio hayo ndio dira ya Chama chetu katika kipindi cha miaka mitano ijayo **(2022 – 2027).** Na ndio yatakayotoa muelekeo wa mradi wa nne wa kuimarisha Chama chetu. Kwa hiyo ni wajibu wa kila ngazi ya Chama, kuandaa **mipango** na **mikakati** ya kufanikisha utekelezaji wa maazimio hayo, katika maeneo yetu.

Aidha, ni wajibu wa Halmashauri Kuu za CCM za ngazi zote, kuanzia Tawi hadi Taifa, kusimamia utekelezaji wa maazimio hayo katika maeneo yao. Hivyo, ninazielekeza Halmashauri Kuu za CCM za ngazi zote, kusimamia kwa karibu na ufanisi utekelezaji wa maazimio hayo katika maeneo yao na kufanya tathmini ya utekelezaji, kila baada ya muda mtakaojipangia, ili kufahamu mafaniko na changamoto zitakazojitokeza na kuandaa mikakati ya kuzipatia ufumbuzi.

Tumeambiwa hapa na Mwenyekiti Mstaafu kwamba, tujue tu ni yepi yatatunyima kura huko mbele. Tukishayajua tunasema utatuzi wake ni upi? Tukishatatua hakuna sababu ya kunyimwa kura huko mbele. Kwa hiyo kazi hii ninayowaagiza kwenda kuifanya itakwenda kulitimiza hilo.

Kwa kuzingatia wajibu wa Chama chetu (**Chama tawala**) na upeo wa majukumu yake kwa Taifa letu, ninashauri kuwa, masuala yafuatayo pamoja na maazimio, yazingatiwe na kuwa **sehemu** ya **maazimio** hayo kama yatakuwa hayajawekwa :

**(1) Kuimarisha Mafunzo ya Siasa, Itikadi na Falsafa ya Chama**

Ujamaa na kujitegemea kwa Mazingira ya sasa. Wenzetu kwenye siasa kama za kwetu wamebadilika sana wamekopa yanayofanyika kwenye siasa za kibepari na kuleta kwetu kuleta kwenye siasa za kijamaa lakini kwa tafsiri nyingine sio ile wanayoiona. Kwa mfano

Wachina wanasema wana ujamaa wa kisasa. Wana sera zao waliozibadilisha huko ndani za ujamaa wa kisasa. Tanzania Vile vile nasi Sera ile ile yetu ya Ujamaa na kujitegemea tunaweza tukaitafsiri kisasa tukaiwekea Sera na tukaitekeleza.

Lakini jengine na Kuimarisha mifumo ya utoaji haki, demokrasia na uongozi bora, tulishafanya Serikalini kama nilivyowaambia tayari nimeunda timu lakini mifumo hiyo ya utoaji haki, demokrasia na uongozi bora inatakiwa pia ndani ya Chama cha Mapinduzi. Kwasababu malalamiko mengi tuliyoyapokea hasa wakati huu wa uchaguzi ni kinyume na utoaji haki, demokrasia na utawala bora.

Kwa hiyo niombe sana Katibu Mkuu na timu yako mjipange vizuri kwenye hili, tumeambiwa walimu wajo wengi hapa, wakina Bashiru, Mkama, Makamba, Mhe. Rais Jakaya, walimu tunao wengi tuwatumie kulifanya hili.

**(2) Kuimarisha uwezo wa CCM na Jumuiya zake na kujenga misingi imara ya uchumi wa kisasa;** Tusibaki CCM ya vibanda vya biashara tu. Vibanda ambavyo nyinyi wa NEC na Wenyeviti wa Miko ana wenzenu mnavichukua kwa shilingi 50 mnakodisha kwa laki mbili. Tusibakie CCM ya vibanda. Twende tukatekeleze miradi mikubwa zaidi. Chama hiki kijitegemee. Uwezo wa kiuchumi wa Chama ndio unanunua uwezo wa kisiasa. Watatokea chama chenye misuli ya fedha waje watupikue. Twendeni tukajiimarisheni. Uwezo wa kiuchumi ndio unashukilia uwezo wa kisiasa.

Na wale ambao wamezoea kula kwa kupitia ngazi za CCM vyeo vya CCM hebu jiulizeni mara tatu kwasababu sasa mfumo wa ukaguzi unakwenda kuimarika.

**(3) Kuimarisha matumizi ya tehama katika matumizi ya Chama chetu;**

**(4) kuimarisha uwezo wa utendaji wa Jumuiya zetu**

Sikubahatika kuhutubia mikutano ya wazazi na vijana wakati wa chaguzi. Lakini nilibahatika kuhutubia mkutano wa UWT na nikawaambia kuna makubwa zaidi mngeweza kufanya kuliko mnayoyafanya sasa hivi. Kwa hiyo twendeni kama chama tunadhamiria na twendeni tukaimarishe uwezo wa Jumuiya zetu. Zisimame Imara ziwe Jumuiya za kutegemewa na sio umuiya ombaomba. Mtapandikiziwa watu. Mtapewa watu lazima muwaweke ambao hawaendani na sifa zenu. Muwe makini kwenye hilo.

Ni Imani yangu kwamba, tukiweza kuyakamilisha haya yote tunayojipangia CCM itakuwa imara zaidi na tutaweza kusimama kama Chama mama kilichozaa wenzetu ambao wanajitahidi kutupa changamoto pale wanapoona kasoro nasi kuzitumia kasoro hizo kufanya marekebisho ili Chama chetu kiendelee kusimama imara.

Ndugu wajumbe mmesikia na kuona utekelezaji wa ILani kwa Serikali zote mbili na mmepata muda wa kujadili utekelezaji wa Ilani hiyo kwa niaba ya wananchi waliowachagua. Ninyi ndio wenye Serikali hizi mbili na nataka muone na mmeona kwa maelezo na

kwa picha kwamba hakuna kilichosimama. Kila mradi, kila eneo, kila pahali, kazi za maendeleo ziko huko zinaendelea.

Hivyo basi, ninyi ndio wenye Serikali msichukue maneno ya pembeni. Tumerudisha dhana ya mshikamano. Kufanya kazi kwa pamoja kati ya Chama na Serikali ili muyaelewe haya.

Muwe na fursa ya kujadili maendeleo yanayofanywa na Serikali yenu. Muwe na fursa ya kutembelea kuona maendeleo maeneo mbalimbali ili wa NEC wajue kitu gani kinafanywa na Serikali yao.

Ili wanapoyasikia nje maneno ya ovyo waweze kujibu na kutetea. Sasa hivi nje kunasemwa maneno ya ovypo na utamkuta mtu wa CCM nae anaongeza uovyo katika hayo hayo. Anajisahau kuwa Serikali inayosemwa ni ya kwake.

Tunakwenda kufanya mageuzi hayo ndani ya Chama ili kukifanya Chama kushika hatamu barabara ya kuendesha Serikali. Tayari tumeshapata safu nzuri za kwenda na kasi ya chama lakini kukabiliana na chaguzi zijazo.

Naomba sasa mnipe baraka zenu nikaipange Serikali kwa jinsi ninavyoona timu hii inaweza kwenda na kuyatekeleza yale tuliyoyapanga hapa kwa vizuri zaidi. Tuliyoyaeleza hap ani utekelezaji wa miaka miwili. Lakini katika safari yangu ya miaka miwili ninahisi kabisa nina watu ambao mwende wao hauendani na kasi yangu. Tunasafari ya miaka mitatu mbele kabla hatujaenda kuwajibishwa kwa wananchi.

Kwa hiyo miaka mitatu iliyobaki, nataka Serikali zote mbili zifanye kazi, tutakapokwenda kwa wananchi tukasimamae na tuwe nay a kuwaambia wananchi. Na kubwa zaidi ni kwamba, tunapokwenda kwa wananchi ni wananchi wenyewe wanaosema Serikali waliyofanya.

Tofauti na utamaduni huko nyuma tulipokuwa tun akwenda kwa wananchi kwamba ni serikali ndio tunawaambia tuliyowafanyia. Twende tukatekeleze ilani ya Uchaguzi. Lakini hata yale mazuri ambayo hayamo ndani ya Ilani ya Uchaguzi lakini tunahisi yatachangia maendeleo ndani ya nchi yetu, tutakwenda kuyatekeleza kama Royal Tour.

Ni muhimu pia kwa Serikali kufanya kazi na kushirikiana ikamilifu na Sekta binafsi. Serikali itaweka mazingira mazuri.

Serikali inaweza kudhibiti uchumi na kudhibiti fedha yetu isishuke na kutoka nje. Ilii tuweze kutekeleza mipango yetu ya maendeleo lazima tukusanye na kulipa kodi. Lazima tuwekeane tozo.

Nimeona hali ya wananchi ni gumu tumeweka ruzuku kwenye mafuta, pembejeo za kilimo na maeneo ya elimu. Fedha za tozo zimejenga shule za msingi na zahanati.

Vikao vya Chama vitaeleza hali za uchumi nah atua tutakazochukua kukabiliana nayo ili muelewe na mkasimame kutetea.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu**

nimalize hotuba yangu kwa mara nyingine tena kuwashukuru sana kwa Imani na heshima kubwa mliyotupa ya kuendelea kutuamini viongozi kuwa kiongozi wa Chama chetu na kutupa **kura nyingi za mafuriko**. Kwa kuwa Imani huzaa Imani, na mimi na wenzangu tunawaahidi **hatutawaangusha!** Kama nilivyoeleza awali, sisi ni watumishi wenu. Ni watumishi wa wananchi wa nchi hii ni watumishi wa watanzania wote. Tuko tayari kuwatumikia kwa nguvu, maarifa na uwezo wetu wote, bila kuchoka bila ubaguzi wa aina yo yote.

Aidha, ninamuomba Molla wetu Mtukufu atupe nguvu na uwezo wa kuyataekeleza hayo kwa ufanisi mkubwa na weledi. Ninachowaomba na kuwasihi Ndugu zangu, ni kutupa **ushirikiano wenu wa dhati** ili tuweze kuyafikia malengo tuliojiwekea na kutimiza matarajio ya wananchi na taifa letu kwa ujumla.
Ndugu zangu baada ya kusema hayo sasa nimalizie kwa kuwatakia safari njema na mkirudi nyumbani Mungu atusimamie wote turudi salama kila mmoja kwa nafasi yake tukateleze tuliyokubaliana.

Na sasa nitamke rasmi kwamba, Mkutano Mkuu wa Kumi wa CCM Taifa, **sasa umefungwa rasmi**.

Nawashukuru Ndugu zangu!

**ASANTENI SANA**